بسم الله الرحمن الرحيم

# MTAZAMO KUHUSU MSUGUANO WA KIMADHEHEBU

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa al-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul Karim Juma Nkusui

**Kimehaririwa na:**
Alhaji Hemedi Lubumba

10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 1 8/19/2013 12:54:23 PM

ترجمة

# رؤية حول السجال المذهبي

تأليف

الشيخ حسن الصفار

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 2 8/19/2013 12:54:23 PM

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN:** 978 - 9987 - 17 - 025 - 8

**Kimeandikwa na:**
Sheikh Hassan Musa al-Saffar

**Kimetarjumiwa na:**
Abdul Karim Juma Nkusui
**Barua pepe:** abdulkarimjuma@yahoo.com

**Kimehaririwa na:**
Al-Haji Hemedi Lubumba Selemani

**Kimepangwa katika Kompyuta na:**
Al-Itrah Foundation

**Toleo la kwanza:** Desemba, 2013
Nakala: 2000

**Kimetolewa na kuchapishwa na:**
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
**Simu:** +255 22 2110640 / 2127555
**Barua Pepe:** alitrah@yahoo.com
**Tovuti:** www.ibn-tv-com
**Katika mtandao:** w.w.w.alitrah.info



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 3 8/19/2013 12:54:23 PM

# YALIYOMO

Neno la Mchapishaji ..................................................... 01

1. Dibaji..................................................... 02

2. Mchango wa majadiliano yenye kuwajibika na msuguano wa kimadhehebu..................................................... 10

3. Kuchangia katika Chanel ya Mustaqilah katika kipindi cha majadiliano ya wazi baina ya Shia na Sunni ..................................................... 19

4. Kuchangia kwa mara ya kwanza..................................................... 19

5. Kuchangia kwa mara ya pili..................................................... 24

6. Kuchangia kwa mara ya tatu ..................................................... 28

7. Je, tofauti za kimadhehebu zinazuia kuoana..................................................... 32

8. Kiambatanisho cha fikira kuhusu majadiliano baina ya Shia na Sunni cha Dr. Khalil bin Abdillahi al-Khalil..................................................... 45



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 5 8/19/2013 12:54:23 PM

10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 6 8/19/2013 12:54:23 PM

# NENO LA MCHAPISHAJI

Mtazamo Kuhusu Msuguano wa Kimadhehebu ni kitabu kinachotoa mwongozo wa jinsi ya kujadiliana katika hali nzuri ya kuamiliana na kuheshimiana baina ya madhehebu na baina ya dini mbalimbali.

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa majadiliano yaliyofanywa na Sheikh Hassan Musa as-Saffar katika kuchangia mjadala uliofanyika katika Channel ya Mustaqilah.

Madhumuni ya mijadala ya Sheikh huyu ni kujaribu kuondoa wingu kubwa lililoigubika mijadala yetu ambayo imekuwa ya kukashifiana, kutukanana, kukufurishana n. k., badala ya kuelimishana, kufahamiana, kuamilana na kujenga umoja wa Waislamu.

Sheikh wetu huyu amechukuwa fursa hii ili kujaribu kuleta muamala mzuri baina ya madhehebu hususan za Kiislamu na dini nyingine kwa ujumla.

Sisi kama wachapishaji tunakiwasilisha kitabu hiki kama kilivyo kwa wasomaji wetu na kuwashauri wasome yaliyomo humo, wayafanyie kazi na kuyazingatia na kufaidika na hazina iliyomo ndani yake.

Hii ni moja kati ya kazi kubwa zilizofanywa na Taasisi ya Al-Itrah katika kuwahudumia kielimu wasomaji wake wazungumzaji wa Kiswahili. Na kwa maana hiyo hiyo imeamua kukichapisha kitabu hiki chenye manufaa makubwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo lake lilelile la kuwahudumia Waislamu hususan wanaozungumza Kiswahili.

Hivyo, ni matumaini yetu kwamba wasomaji wetu watanufai-



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 1 8/19/2013 12:54:23 PM

ka vya kutosha kutokana na kitabu hiki, kwani tumekiona ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote ambapo uwongo, ngano za kale na upotoshaji wa historia na kugombanishwa wenyewe kwa wenyewe ni vitu ambavyo havina nafasi tena katika akili za watu.

Tunamshukuru mwandishi wa kitabu hiki, Sheikh Hassan Musa al-Saffar kwa kazi kubwa aliyofanya kwa ajili ya Umma huu wa Waislamu, Allah 'Azza wa Jallah amlipe kila la kheri na amuingize Peponi kwa salama na amani insha'Allah. Halikadhalika tunamshukuru ndugu yetu Abdul Karim Juma Nkusui kwa kukitarjumi kwa Kiswahili kitabu hiki, insha'Allah na yeye Allah 'Azza wa Jallah amlipe kila kheri hapa duniani na Akhera pia, bila kuwasahau na wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine mpaka kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na huko Akhera.

**Mchapishaji**
**Al-Itrah Foundation.**



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 2 8/19/2013 12:54:23 PM

# DIBAJI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

إِنَّ هَٰذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُونِ

**"Hakika umma wenu huu ni umma mmoja, na mimi ni Mola Wenu kwa hivyo niabuduni."** **(Surat Anbiyai: 92).**

Sifa zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe, rehema na amani zimwendee kipenzi chetu Mtukufu wa daraja Mtume Muhammad (saww), kizazi chake kitukufu na Masahaba wake wema.

Ama baad, Waislamu leo wanaishi katika hali yenye kukabiliwa na changamoto nyingi sana, na moja ya changamoto hizi ni muamala na uhusiano mbaya baina ya madhehebu za Kiislamu. Suala la muamala mzuri na mahusiano mazuri katika jamii ya kibinadamu ni muhimu sana katika maisha ya kila siku, kwa sababu binadamu kama binadamu ni lazima aamiliane na binadamu wenzake kwa hali yoyote ile, kwani maisha hayatimii bila ya kufanya hivyo, kila mtu kwa namna moja au nyingine anamhitaji mwingine ili kufanikisha na kuendesha maisha yake. Hivyo hata bila ya kuwa na dini binadamu analazimika kuwa na muamala mzuri na watu wengine ili aweze kuishi vizuri hapa duniani. Duniani kuna wafuasi wa dini mbalimbali sawa iwe ni ile inayotambuliwa na kukubalika kwa Mwenyezi Mungu au nyinginezo. Wote hawa wanapasa kuheshimiwa na kupata muamala mzuri kwa binadamu wenzao kama binadamu.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 3 8/19/2013 12:54:23 PM

Uislamu ni dini ambayo anaikubali Mwenyezi Mungu na kwamba ndio dini pekee ambayo kama mwanadamu atamwendea Mwenyezi Mungu na dini nyingine isiyokuwa Uislamu atakuwa amepata hasara na hatokubaliwa kabisa, na amali zake zote zitakuwa zimepotea bure, na hiyo ndio hasara kubwa kabisa.

Lakini Uislamu unatambua uwepo wa watu wengine ambao ama mila zao na dini zao hazikubaliani na Uislamu au zinapingana kabisa na dini ya Kiislamu, lakini pamoja na hivyo Uislamu umewataka Waislamu wawe na muamala mzuri pamoja nao, na wanapotaka kuzungumza nao kwa hoja au kujadiliana nao, Uislamu umeelekeza kwamba mazungumzo yao na mjadala wao utawaliwe na lugha nzuri, uelewano mzuri, hekima na busara kubwa. Anasema Mwenyezi Mungu (swt):

قُلْ يَا أَهْلَ الْكِتَابِ تَعَالَوْا إِلَىٰ كَلِمَةٍ سَوَاءٍ بَيْنَنَا وَبَيْنَكُمْ أَلَّا نَعْبُدَ إِلَّا اللَّهَ وَلَا نُشْرِكَ بِهِ شَيْئًا وَلَا يَتَّخِذَ بَعْضُنَا بَعْضًا أَرْبَابًا مِنْ دُونِ اللَّهِ ۚ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُولُوا اشْهَدُوا بِأَنَّا مُسْلِمُونَ

**“Sema: Enyi watu wa Kitabu! Njooni kwenye neno la usawa baina yetu na baina yenu. Kwamba tusimwabudu yoyote ila Mwenyezi Mungu, wala tusimshirikishe na chochote; wala baadhi yetu wasiwafanye baadhi kuwa waungu zaidi ya Mwenyezi Mungu. Wakikataa, semeni: Shuhudieni ya kuwa sisi ni Waislamu.” (Surat Aali Imran: 64).**

Tunafundishwa kupitia Aya hii tukufu kwamba mazungumzo na watu wa dini zingine ni muhimu yafanyike katika njia nzuri ya adabu na heshima ya hali ya juu, kwani ni kwa namna hii tu, ndio tunaweza kuwavutia watu na kuwakinaisha na hatimaye kufikia lengo letu la



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 4 8/19/2013 12:54:24 PM

kuwaita katika njia ya Mwenyezi Mungu. Lugha nzuri, tabia nzuri, muamala mzuri, hekima na busara ndio zinatakiwa zitawale mjadala na mazunguzo ya kulingania kwa Mwenyezi Mungu.

Lakini kwa kuwa katika mazungumzo inawezakana isipatikane natija nzuri ya kufikia mwafaka, basi hata hilo litakapotokea basi hiyo haimaanishi kufungua mlango wa muamala mbaya, matusi na sintofahamu, bali muamala mzuri lazima uendelee na wala hilo lisiwe ni chanzo cha chuki, bughudha na kadhalika. Kwani hawa bado watakuwa ni wenzetu katika ubinadamu. Imamu Ali (as) anatuambia: "Watu wako aina mbili: Ndugu yako katika dini au ni mwenzako katika maumbile." Mwanadamu hata kama sio ndugu yako katika dini bado atabakia kuwa ni binadamu katika maumbile, ni binadamu kama wewe.

Mtume wetu (saww) katika Hadithi mashuhuri kabisa ametuambia kwamba: "Mayahudi wamegawanyika makundi sabini na moja, na Manaswara wamegawanyika makundi sabini na mbili, na umma huu utagawanyika makundi sabini na tatu, yote yatakwenda motoni isipokuwa kundi moja tu." Sina shaka kwamba katika makundi yote haya kila moja linadai kuwa lenyewe ndio hilo kundi moja lililobashiriwa pepo na Mtukufu Mtume (saww). Pamoja na hivyo makundi yote haya ni makundi ya Kiislamu na yanaunganishwa na kalimat "Laa Ilaaha illa llahu Muhammadu Rasulullahi. Hivyo yote hayo ni makundi ya Kiislamu.

Pia hakuna shaka kwamba kila kundi au madhehebu linalingania katika madhehebu yake na kutafuta wafuasi, na hili ni jambo la kawaida na halihitaji maelezo mengi kulithibitisha.

Suala la msingi hapa ni namna gani makundi haya pamoja na wingi wake na mgawanyiko wake yanatakiwa yaishi, na ni jinsi gani wafuasi wa kundi moja waamiliane na makundi mengine au



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 5 8/19/2013 12:54:24 PM

madhehebu mengine. Hili ndio la muhimu sana. **"Lingania katika njia ya Mola Wako kwa njia iliyo nzuri na hekima."** Tofauti za madhehebu ya Kiislamu zilizo nyingi ziko katika mambo ya matawi na sio ya msingi. Hivyo kuna mambo mengi sana ya msingi yanayounganisha madhehebu yote haya ya Kiislamu.

Na suala hili tukiliangalia kwa makini ni suala ambalo limetokana na tofauti za kifikra na uwelewa katika baadhi ya nususi za Qur'ani na Sunnah, jambo ambalo halikwepeki kwani kila mtu ana akili yake, kwani "Akili ni nywele na kila mtu ana zake." Na upeo wa kufikiri na kuelewa unatofautiana kati ya mtu na mtu. Hata katika madhehebu moja watu wanatofautiana hawako katika fikra moja pamoja na kwamba wanaafikiana katika misingi, hata mwalimu pia anaweza kutofautina na mwanafunzi wake ambaye ametaabika kumfundisha na kumwandaa kwa muda mrefu, kwa sababu kila mtu ana upeo wake wa kufikiri.

Sio jambo la kushangaza mtu kusoma katika vitabu vya madhehebu moja na kuona Maulamaa wanatofautiana na pengine kukufurishana kutokana na tofauti za uwelewa juu ya mas'ala fulani ambayo huyu ameelewa hivi na yule ameelewa vile, na hivyo kila mtu akatoka na mtazamo wake uliotofauti na wa mwenzake. Mwenyezi Mungu alipotufundisha juu ya muamala mzuri na watu wengine wasiokuwa Waislamu na kwamba tuongee nao kwa heshima, hekima na busara, hii inamaanisha kwamba sisi ndio aula wa kuyafanya haya baina yetu, baina ya madhehebu zetu ambazo zote ni za Kiislamu na zote zinasema "**Laa ilaaha illallah Muhammadu Rasullullahi.**" Mazungumzo yetu lazima yatawaliwe na lugha nzuri ya heshima, ya uwelewano, hekima na busara kubwa, kwa sababu sote tupo katika duara moja na nyumba moja, kila utakapombomoa mwenzako basi utakuwa unaibomoa nafsi yako na dini yako, na mwisho wa siku wewe mwenyewe ndio utakayepata hasara kwa kujidhoofisha mwe-



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 6 8/19/2013 12:54:24 PM

nyewe na kutoa fursa nzuri kwa maadui zako, ambao wanaisubiria kwa hamu kubwa fursa hiyo.

Sisi Waislamu ni ndugu, ni jengo moja, na ni kiwiliwili kimoja ambacho kinapougua kiungo lazima mwili wote uugue na ukeshe kwa homa, maumivu, adha na taabu, ni lazima muamala wetu uwe ni bora zaidi, uwelewano zaidi, kufahamiana na ushirikianao kuliko muamala wetu na watu wengine ambao tunatofautina nao katika dini.

La ajabu na la kushangaza ni kuona muamala baina yetu ni mbaya mno kiasi kwamba anayeangalia kwa nje hawezi kuamini kuwa hawa ni watu wa dini moja, kibla kimoja, watu wanaomwamini Mwenyezi Mungu Mmoja, Mtume wao ni mmoja na Kitabu chao ni kimoja, ni ajabu kabisa hali hii. Mtu anamaliza kutukana na kuwakufurisha ndugu zake Waislamu kisha anasimamisha Swala hali ya kuwa Swala yake haimkatazi kumtukana ndugu yake, kumkufurisha Mwislamu mwenzake. Je, kumtukana Mwislamu si ufasiki, je kumkufurisha Mwislamu mwenzako si ukafiri?

Tunafundishwa kwamba tunapozozana na kuhitalifiana turejee katika Kitabu na Sunnah sio kwenye matusi na kukufurishana. Waislamu bado tuna fursa nzuri ya kurekebisha hali hii na hata kuimaliza kabisa, lakini lazima watu wasafishe nia zao na muamala wao, busara na hekima zitawale katika muamala wao, ndimi zao ziwe laini kwa dhikiri ya Mwenyezi Mungu na sio kwa matusi na kuwakufurisha Waislamu wenzao.

Uvumilivu pia ni kati ya mambo ambayo leo hii yanawashinda watu wengi, ni mara ngapi tunashuhudia maneno na lugha mbaya ya kutukanana baina ya Masheikh wawili waliokuwa wanaswali msikiti mmoja, eti kwa sababu moja au nyingine anapoondolewa katika uongozi au kwa kutokuelewana, mmoja anafungua msikiti wake



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 7 8/19/2013 12:54:24 PM

na kisha kufungua mlango wa matusi na mashambulizi bila ya aibu wala adabu wala haya kwa Sheikh mwenzake, na hata kumkufurisha, na mifano iko chungu nzima baina ya madhehebu moja achilia mbali baina ya madhehebu mbili.

Tunajua wazi kwamba katika kila madhehebu kuna watu wenye jazba na hamasa kupita kiasi, ila la msingi ni kudhibiti yote hayo ili tuweze kurejea katika hali nzuri ya uwelewano kwa kujali mambo ya msingi yanayotuunganisha na kutufanya tuwe wamoja, kwani vitabu vyetu sote vimekokoteza mambo mengi, yaliyoandikwa ni mengi mno kutoka katika kila pande na wala hakuna yeyote anayethubutu kusema vitabu vya upande wake vimeepukana na hayo hata kama hayakubaliki na kwamba yamekuja kwa mapokezi dhaifu lakini yapo.

Njia iliyopo ni kurejea katika uongofu wetu, muamala mzuri, tusome vitabu vyetu tuangalie yanayotuunganisha na tuepukane na yanayotufarakisha ili tuweze kufikia lengo letu kwa urahisi.

Mwandishi wa kitabu hiki ni kati ya Maulamaa na wanaharakati ambao wamefanya jitihada na wametoa juhudi nyingi, ambao wanaona kwamba kuna haja mijadala yetu na midahalo yetu iwe na sura na mwelekeo wa uwelewano na kufahamiana, na kila upande ujue upande mwingine, mjadala sio uwanja wa ushindani wa kimadhehebu, wala sio mahakama kwa upande mmoja kuutia hatiani upande mwingine, wala sio uwanja wa kila mtu kuonyesha uwezo wake na uhodari wake kwa njia isiyofaa, mjadala sio vita baina ya wanamadhehebu, mjadala ni jukwaa la kuelewana na kutafiti mambo yanayotuunganisha na kutufanya tuwe wamoja, kujua kasoro ili tuziepuke na kutafuta mazuri ya kutuleta pamoja ili tuyafuate.

Ni kwa njia hii tu, ndio tunaweza kuunusuru ummah na hali hii mbaya ambayo inatunyemelea na ambayo inapigiwa dede na wa-



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 8 8/19/2013 12:54:24 PM

sioutakia mema ummah wa Kiislamu, kwani furaha yao ni kutuona tunaparaganyika na kusambaratika ili wao wafikie malengo yao kiurahisi na hatimaye kutufanya watumwa wao. Ama kweli vita vya panzi ni furaha ya kunguru.

Zifuatazo ni baadhi tu ya nukta na mchango wa Sheikh huyu, ambao aliutoa miaka michache iliyopita katika kuchangia mjadala uliofanyika katika Chanel ya Mustaqilah na kisha mchango huo ukawekwa katika njia ya maandishi ili faida iwe kubwa zaidi na iwafikie watu wengi zaidi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atie tawfiki kupitia kitabu hiki na kuunusuru ummah kutokana na mparaganyiko, Naye Ndiye Mwenye kuombwa msaada.

**Abdul-Karim J. Nkusui - Mtarjuma**



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 9 8/19/2013 12:54:24 PM

بسم الله الرحمن الرحيم

# MAJADILIANO YENYE KUWAJIBIKA, NA MSUGUANO WA KIMADHEHEBU

Wakati huu ambao unaupitia ummah wetu wa Kiislam ndio wakati mgumu sana na hatari mno. Haijatokea ummah kukabiliana na changamoto za kina na za hatari kama unavyokabiliwa katika wakati uliopo. Ni sahihi kwamba ummah ulipitiwa na nyakati ngumu ambapo uliishi katika hali ya kuporomoka na kushindwa, lakini yanayotokea sasa hivi ni ya hatari mno na magumu sana, ambapo ummah unakabiliwa na changamoto kali sana za nje, na changamoto kali sana za ndani. Ama kuhusu changamoto za nje, ni kwamba hakika iliyo wazi kabisa ni nguvu kubwa ambayo inatawala ulimwengu leo, ambayo ni Marekani, inaongoza vita, mapambano na ugomvi dhidi ya ummah wa Kiislamu, hivyo inatumia na inatayarisha kila nguvu ya ulimwengu ikiwemo taasisi za kimataifa kama vile Baraza la Usalama, Umoja wa Mataifa na nyinginezo, kupigana vita dhidi ya Uislamu na Waislamu.

Ni sahihi kwamba viongozi wa Marekani wanasema vita yao na mapambano yao si dhidi ya Uislamu na Waislamu, bali ni dhidi ya magaidi tu, lakini hali ambayo inaendelea duniani na ushahidi tunaouona unaonyesha kwamba Marekani inaishi katika hali ya kivita ya wazi dhidi ya Uislamu katika wigo na nyanja mbalimbali. Na kati ya ushahidi unaojitokeza zaidi ni haya matamko makali makali dhidi ya Uislamu na Waislamu yanayotolewa kwa njia ya vyombo vya habari. Ndani ya mwaka huu vimetoka vitabu na mihadhara mingi ya kimasomo inayoutukana Uislamu na



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 10 8/19/2013 12:54:24 PM

Waislamu. Kwa mfano tu vyombo vya habari vimenukuu maneno ya mmoja wa viongozi wa utamaduni katika nchi za Magharibi, naye ni mwandishi wa Kiingereza "Napole" ambaye amepewa tuzo ya Nobel ya fasihi mwaka huu, kwamba amesema: "Waislamu wamejawa na chuki na wala hawakubali kuishi pamoja na wengine. Na Waarabu ni ummah wa wajinga, hausomi na unasimama dhidi ya maendeleo." Amesema maneno haya katika siku ambayo alipokea tuzo ya Nobel.

Ama mwandishi wa kike wa Kiingereza Palatshiy ambaye amesifiwa na Waziri wa zamani wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani "Henery Kisinjer" kwamba yeye ni mwerevu zaidi na ni mwandishi bora zaidi ulimwenguni, aliandika kitabu ambacho humo amesema: "Hakika Waislamu wote, kwa ujumla wao pamoja na uzuri wa hali zao, hawana uadilifu, na kwamba nyuma ya hali hii ya ukosefu wa uadilifu yupo Muhammad na Qur'ani yake." Na kinapotoka kitabu hiki mamilioni ya nakala zinauzwa.

Na mtangazaji wa kike maarufu na mashuhuri wa Kimarekani Loura anasema: "Hakika Waislamu ni ummah unaolea watoto wao katika umri wa mwaka wa pili na wa tatu namna ya kuuwa makafiri (yaani wasiokuwa Waislamu)." Na ulimwengu ulisikia maneno hayo aliyoyasema Kasisi maarufu wa Marekani juu ya Mtume (saww) pale alipomwelezea kwamba ni gaidi mkubwa katika historia. Hakika maneno haya na mfano wake hakika ni moja ya aina za vita na mapambano dhidi ya Uislamu na Waislamu.

Katika upande mwingine Wamarekani wanaamiliana pamoja na Mwislamu katika nyanja mbalimbali duniani kwa kumzingatia kuwa ni mtu mwenye kushukiwa na mahala pa shaka, na vyombo rasmi vya Serikali ya Marekani vinatoa kanuni zinazopelekea kuchukuliwa hatua maalum dhidi ya wananchi wa nchi za Kiislamu. Wao ni duni kuliko wengine, wanapekuliwa kwa umakini na ku-



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 11 8/19/2013 12:54:24 PM

zuiwa kwa muda mrefu na wanahojiwa bila ya kuchunga haki wala mipaka, na yote hayo kwa hoja ya kuupiga vita ugaidi.

Ama taasisi za elimu au za kiuchumi za Kiislamu hakika zinakabiliwa na kibano kikali kutoka kwa Wamarekani kwani mali nyingi za taasisi za kheri zimezuiliwa, na zimezuiliwa kufanya shughuli zao kwa hoja ya kusaidia ugaidi.

Ama ambayo tunayaona leo miongoni mwa sura inayojitokeza kwa ndugu zetu wa Kipalestina huko Palestina, kwa kuiacha huru mikono ya Mazayuni ili ichezee na kuharibu kila kinachomilikiwa na Wapalestina ambapo Sharon (Nentanyahu na wengineo) anateka miji na anavunja nyumba na anauwa watoto na wanawake, na anaharibu mashamba na mali mbele ya macho na masikio (ya watu) bali mbele ya ulinzi wa Marekani, pia ni ushahidi mwingine unaothibitisha kwamba yanayotokea si kingine isipokuwa ni vita dhidi ya Waislamu, kwa kuanzia na ardhi tukufu ya Palestina. Na anapotaka mmoja kati ya Wapalestina kufanya hayo Wamarekani wanamzingatia kuwa ni gaidi.

Kama ambavyo leo hii Marekani inaizingatia kila nchi ya Kiarabu na ya Kiislamu kuwa ni uwanja ulio wazi wa shughuli zake za kijeshi na wanatishia kuzigawa nchi za Kiarabu na za Kiislamu, na kuchora upya ramani yake.

## CHANGAMOTO ZA NDANI

Na inaonekana changamoto ya ndani ya kubaki nyuma zaidi kimaendeleo ambayo ummah wa Kiislamu unaishi nayo, ni hatari zaidi kuliko changamoto za nje, bali ndio iliyofungua mlango mbele ya changamoto za nje. Kama sio kutokuendelea kwetu, basi maadui wasingekuwa na ujasiri dhidi yetu, na kama sio kufeli kwetu mambo yasingekuwa katika hali hii ambayo tumo leo.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 12 8/19/2013 12:54:24 PM

Inatosha kusoma ripoti ya maendeleo ambayo imetolewa na sanduku la mpango wa maendeleo wa Umoja wa Mataifa wa mwaka 2002, kuhusu kumwendeleza mwanadamu mwarabu. Katika ripoti hii kuna matukio ya kushangaza juu ya hali ambayo ummah wa Kiarabu unaishi, ambapo idadi ya Waarabu inafikia milioni 280 waliotawanyika katika nchi 22, nayo inazidi idadi ya wananchi wa Marekani ambao hawazidi milioni 265.

Ripoti inazungumzia juu ya uzalishaji wa jumla wa nchi za Kiarabu na ambao unafikia kwa mwaka mmoja tu dola bilioni 531, wakati tunakuta nchi ya Ulaya ya kawaida kama vile Hispania uzalishaji wake unafikia dola bilioni 595. Na wastani wa ukuaji wa pato la mwananchi wa nchi ya Kiarabu kwa mwaka ni 5.0 hivyo ili liongezeke pato la mwananchi wa nchi ya Kiarabu anahitaji miaka 140 wakati ambapo mwananchi wa nchi zilizoendelea anahitaji miaka 10 ili kuongezeka pato lake. Na kuna Waarabu milioni 65 watu wazima wasiojua kusoma na kuandika, theluthi mbili ya idadi hii ni wanawake, kama ambavyo kuna milioni 10 ya watoto wa Kiarabu walio katika umri wa kusoma lakini hawako shule, na idadi ya wasio na kazi ni milioni 12, na kiwango cha wanaojiunga na masomo ya juu kwa ajili ya kukamilisha masomo yao ni asilimia 13 tu, wakati ambapo idadi ya watu hawa katika nchi za viwanda inafikia asilimia 60.

Na katika ripoti nyingine ya Unesco ni kwamba hakika idadi ya tafiti za kielimu zilizochapishwa na kusambazwa katika nchi za Kiarabu na za Kiislamu mwaka 1993, ziliwakilisha asilimia moja tu ya jumla ya tafiti zilizosambazwa katika nyanja zote za maarifa. Na ripoti inaonyesha kwamba idadi ya watafiti katika nchi ya Kiarabu ni watafiti elfu 8, wakati ambapo tunakuta Israil ina watafiti eflu 40 wa elimu, pamoja na kujua kwamba idadi ya wakazi wake hawazidi milioni 5.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 13 8/19/2013 12:54:24 PM

Hakika sisi katika kupambana na changamoto tunahitaji mambo mawili:

**Kwanza:** Kutafakari katika namna ya kupambana na changamoto hizi. Hakika jukumu la kwanza ambalo ni wajibu tuishi nalo na tulipe kipaumbele ni namna ya kupambana na changamoto hizi za ndani na za nje, na kwa ajili ya hilo ni wajibu tufanye kongamano na tupange majadiliano na tutoe juhudi, kwa sababu akili inaamuru hivyo, maadamu mwanadamu anakabiliwa na hatari, basi ni juu yake atafakari namna ya kukabiliana nazo na kuzishinda.

**Pili:** Kuunganisha idara za ummah na kupanga safu zake ili kuvuka changamoto hizo, kwa sababu hatari itatutishia sote.

## USHINDANI WA MAKUNDI

Lakini tunapata nini katika hali ya ummah?

Je, kuna harakati za kuunganisha nguvu ya ummah na vipaji vyake ili kupambana na changamoto? Yana nafasi ipi mbele ya changamoto zote hizo yale tunayoyaona katika baadhi ya Chanel katika siku hizi miongoni mwa mijadala ya kimadhehebu?

Badala ya ummah kushughulika na kupambana na mambo yake na matatizo yake ya msingi unatumia nguvu zake katika mijadala ya kimadhehebu na kimakundi, mijadala inayovutia mazingatio ya wengi kati ya watu wa ummah, na ambao ni wepesi kukubali mfano wa mambo kama haya, hiyo ni kwa sababu mazingatio mengine alama zake haziko wazi katika akili zao. Na hivyo utaona majilisi na klabu zinashughulika na tofauti za kimadhehebu zisizo na matunda. Hakuna ratiba zinazozungumzia juu ya mbinu za maendeleo, na namna gani ummah utavuka hali ya kushindwa na kufeli ambayo



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 14 8/19/2013 12:54:24 PM

unaishi nayo, hakuna ratiba ambayo inapanga na kushauri rai na fikira juu ya kuunganisha nguvu za ummah na juhudi zake, bali ni ratiba inayourejesha ummah nyuma na kushughulika na ikhitilafu zilizopita na hata kushughulika na mijadala ya kimadhehebu isiyo na matunda. Ni kitu gani hiki kinachotokea? Kwa nini katika wakati huu harakati za kimadhehebu zimepamba moto?

Vitabu vinasambazwa ili kuchochea moto wa fitina za kimadhehebu na fatwa zinazungumza kwamba inajuzu Mwislamu kumuoa mkristo na myahudi, lakini haijuzu kumuozesha Shia, kulingana na maneno yao. Wanahamasisha, na hamasa hii pia utaikuta inachochewa na Mashia kwa kutoa vitabu na makala kwenye tovuti vinavyochochea ghadhabu kwa ndugu zao Masuni. Wanataka nini kwa ratiba kama hizi? Juhudi hizi zinataka nini? Baadhi ya magazeti na taasisi huko Marekani zinazungumzia juu ya kuzigawa zaidi nchi za Kiarabu hata Makka na Madina.

Kisha wanakuja baadhi ya wasio waadilifu ili kuchochea fitina hizi za kimadhehebu, je hayo hayaonyeshi kwamba juhudi hizi na kazi hizi ni miongoni mwa mpango wa maadui ili kuusambaratisha ummah huu?

Maadui wanapozungumzia kugawa na kusambaratisha ummah huu ni lazima watengeneze mazingira na waandae hali ya mgawanyiko huu na usambaratishaji huu, na hiyo ni kwa kuchochea mizozo ya utaifa na kiukoo, kimadhehebu na kimakundi, hali hii ndio mazingira wanayoyataka maadui ili watekeleze mbinu zao za kugawanya.

Na katika upande mwingine Uislamu unatuhumiwa na Wamagharibi kuwa unahamasisha chuki, na unalea uadui na unalea watoto wake juu ya kutaoamiliana pamoja na wengine na wala haukubali rai za wengine, na Waislamu wanapambana ili kujibu tuhuma hii na kuusafisha



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 15 8/19/2013 12:54:24 PM

Uislamu na hayo. Katika nchi ya Saudia imetoka taarifa inayoelekezwa kwa wasomi wa Kimarekani, taarifa ambayo imetiwa saini na baadhi ya maulamaa wa Saudia na wanafikira wake wakijibu tuhuma hii iliyo dhidi ya Uislamu. Nani anasema kwamba Uislamu unahamasisha chuki, bali Uislamu ni dini ya majadiliano na ni dini ya usamehevu, na kwa nia njema kabisa ulifanywa mkutano huko Riyadh kuhusu majadiliano juu ya tamaduni, kwa ajili ya kuthibitisha kwamba Uislamu unakaribisha mazungumzo pamoja na tamaduni nyingine, na kwamba katika Uislamu kuna usamehevu unaowaenea watu wengine.

Lakini itakuwaje, ikiwa Wamagharibi wataona, na wao wanaangalia vipindi hivi ambavyo vinarushwa kuhusu mijadala ya Kimadhehebu? Na namna gani huyu akimshambulia yule na kumwambia: "Wewe ni kafiri, wewe ni zandiki, wewe ni mnafiki, wewe ni kadha wa kadha?" Je, huku si kusadikisha madai na maneno ambayo wanayasema dhidi ya Uislamu na Waislamu? Je, si haki kwa Wamagharibi kusema: "Tazameni Waislamu, sio tu wanahamasisha chuki dhidi ya wanaowakhalifu katika dini; ndani yao pia hawawezi kuishi na wenzao, kwa sababu wao wanawalea watoto wao juu ya chuki ya kuchukiana wao kwa wao."

Hivyo maneno haya ambayo wanayasema Wamagharibi kwamba Uislamu unalea watoto wake juu ya chuki na mifundo, yanapewa usadikisho na uthibitisho na kundi hili lenye kushabikia umadhehebu. Na hakika mpasuko huu wa kimakundi hakika unatumikia madai ya maadui dhidi ya Uislamu. Hadi lini ummah huu utaishi katika hali hii? Sisi hatupingi majadiliano, Waislamu wajadiliane katika madhehebu yao mbalimbali na kila mmoja atoe rai yake na wajadiliane, kwani majadiliano, midahalo na mazungumzo ya kielimu ni jambo zuri, lakini kuna mambo mawili:

**Kwanza:** Kuhusu wakati wa mjadala huu, je, huu ni wakati wa kutafiti mambo haya? Je, ummah hivi sasa una nafasi ya mjadala



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 16 8/19/2013 12:54:24 PM

huu? Maadui hivi sasa, na wao wanapanga mikakati ya kuipiga Iraki, na wanatishia nchi zilizobakia za Kiarabu na za Kiislamu, na Sharon anataka kufanya mashambulizi makali katika ardhi ya Palestina, huku hali iliyomo ndani ya jamii yao ni kuwa watakabilina na ghadhabu katika mitaa ya Kiarabu na ya Kiislamu. Lakini midahalo hii, na vipindi hivi vinawaambia Wamarekani na Mazayuni kwamba mitaa ya Kiarabu na Kiislamu inashughulika na mijadala na midahalo isiyo na faida.

Hakika manowari za Kimarekani za kijeshi zimejaa katika sehemu zetu na viongozi wake wanatishia kila siku kwa kusogeza vikosi vyao vya askari Iraki, na ambavyo vinaitishia nchi kwa hatari kubwa dhidi ya utulivu wake wa kisiasa na hali yake ya kiuchumi, na mustakabli wake wa kijamii, kama ambavyo Sharon (Nentanyahu kwa sasa) anaendeleza mkakati wake wa kuwashambulia wananchi wa Palestina bila ya woga wowote. Je, huu ndio wakati unaofaa kutafiti mambo haya?

**Jambo la pili**: Hili linahusiana na mbinu za mjadala na njia yake, je huu ni mdahalo wa kielimu?

**Je, ni mjadala wa kimantiki?**

Yanayotokea katika mijadala hiyo ni matusi na mashambulizi ambayo hayalandani na mwanadamu Mwislamu, hakika Qur'ani inatuamuru kuwa majadiliano pamoja na wasiokuwa Waislamu yawe kwa njia bora zaidi, na kwa daraja la juu la adabu na hekima, anasema (swt):

وَلَا تُجَادِلُوا أَهْلَ الْكِتَابِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِلَّا الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 17 8/19/2013 12:54:24 PM

**"Wala usijadiliane na watu wa Kitabu isipokuwa kwa njia iliyo nzuri kabisa; isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao."** **(Surat An'kabut: 46).**

Na anatuamuru kutegemea dalili na hoja katika majadiliano:

قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ صَادِقِينَ

**"Sema: Leteni dalili zenu kama nyinyi ni wasema kweli."** **(Surat Baqarah: 111).**

Na amesema:

قُلْ هَلْ عِنْدَكُمْ مِنْ عِلْمٍ فَتُخْرِجُوهُ لَنَا ۖ إِنْ تَتَّبِعُونَ إِلَّا الظَّنَّ وَإِنْ أَنْتُمْ إِلَّا تَخْرُصُونَ

**"Je, mnayo elimu mtutolee? Nyinyi hamfuati ila dhana tu, na hamsemi ila uwongo tu."** **(Surat An'am: 148).**

Majadiliano yanapasa yawe ya kielimu na sio matusi. Huu ni mushkeli wa kimadhehebu ambao baadhi ya jamii za Kiislamu zinaishi nao, inapasa kwa viongozi wa ummah, serikali, maulamaa na watambuzi wa mambo watafakari katika kuuvuka, au kwa uchache kuudumaza.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 18 8/19/2013 12:54:24 PM

# KUCHANGIA KATIKA CHANEL YA MUSTAQILAH KATIKA KIPINDI CHA MJADALA WA WAZI BAINA YA SHIA NA SUNNI

## KUCHANGIA KWA MARA YA KWANZA:[1]

Hakika mjadala baina ya Waislamu, hususan katika wakati huu hatari na mgumu, inapasa uwe ni hatua moja katika njia ya ummah huu kuvuka matatizo ya kutokuendelea ambayo ummah unaishi nayo.

**Kutokuendelea ambako kunajikita katika pande mbili:**

Upande wa kwanza: Kutokuendelea kielimu, ambapo hakuna nafasi ya ummah mpana wa Kiislamu inayotajwa katika nyanja ya mafanikio ya kielimu ya binadamu, nafasi ya nchi za Kiislamu, kwa maelfu ya mamilioni ya raia wake, haivuki asilimia moja katika utafiti wa kielimu uliosambazwa katika matawi yote ya elimu na maarifa, kama ilivyokuja katika sensa ya Unesco ya mwaka 1993.

Upande wa pili: Kutokuendelea katika nyanja za uhusiano, ambapo hali ya ummah kwa ndani inakabiliwa na mkaganyiko katika upande wa kisiasa na upande wa kidini, uhusiano baina ya serikali za Kiarabu na za Kiislamu sio mzuri, kama ambavyo ni maarufu, na vilevile baina ya serikali nyingi na wananchi wake, na baina ya harakati na nguvu za kisiasa, katika ulimwengu wa Kiarabu na wa Kiislamu.

[1] Ilikuwa usiku wa Ijumaa mwezi 20 Dhul-Qaad 1423 sawa na 23 Januari, 2003.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 19 8/19/2013 12:54:24 PM

Na katika upande wa kidini kuna msuguano huu mbaya wa kimadhehebu na kimakundi, ambao tumeona sehemu ya mwonekano wake kupitia mazungumzo ya midahalo iliyotangulia katika mwezi wa Ramadhani katika Chanel ya Mustaqilah, na ndani ya kila kundi na madhehebu pia kuna ikhtilafu na aina za mgongano na mizozo, kama tulivyoona namna gani mtu amepiga simu akimtukana Sheikh al-Khaaliswiy na shule ambayo anaiwakilisha kwa upande wa Shia, na vilevile jibu la Sheikh al-Khaaliswiy kwake. Vivyo hivyo ndani ya Sunni, kunapatikana mfano wa msuguano huu. Hakika msuguano huu wa kisiasa na kidini unaakisi hali ya kushindwa na kutoendelea katika uwelewa wa kimaisha, na katika uwezo wa kuamiliana na hali ya kuhitalifiana na kutofautiana.

Hivyo ni lazima kuwepo na mjadala wa wazi na huru ili kuvuka hali hii ya kutoendelea, na matatizo haya ya kimaisha. Hakika utamaduni wetu wa Kiislamu hivi sasa umetuhumiwa ulimwenguni, na hususan baada ya tukio la Septemba 11 kwamba una kasumba na unaunga mkono ugaidi na ubabe. Na wenye ikhilasi katika ummah huu wanapigana ili kuonyesha upole wa Uislamu na mafunzo yake katika kumheshimu mwanadamu na kuamiliana baina ya jinsia ya kibinadamu. Lakini hali ya msuguano na mizozo ya ndani baina ya pande zenye nguvu na madhehebu, unafuta juhudi zote hizi zenye ikhilasi, ambapo ni namna gani tutawakinaisha wengine wasiokuwa Waislamu kuwa tuna utayari wa kuamiliana nao kwa kuheshimu haki zao ilihali tunashindwa kuamiliana kwa heshima baina yetu? Na namna gani tutawakinaisha wengine kwamba sisi tuko tayari kukubali rai ya mwingine na kuamiliana na dini zingine na binadamu wengine kwa heshima?

Hakika mimi naunga mkono, tena kwa nguvu, aliyoyatoa Dr. Khalil bin Abdillah al-Khalil mjumbe wa bodi ya ukufunzi katika Chuo Kikuu cha Imam Muhammad bin Suud al-Islamiyyah kwam-



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 20 8/19/2013 12:54:24 PM

ba uwasilishaji uwe ni uwasilishaji wa uwelewa na wa uhalisia. Na naona kwamba mjadala ni wajibu uwe ni kwa ajili ya kujuana kwa usahihi, kila kundi lifahamu lile lililonalo kundi jingine kupitia katika rejea zake na kupitia rai inayokubalika kwake.

Tumeona mazungumzo yaliyotangulia katika Chanel ya Mustaqilah katika mwezi wa Ramadhani, namna gani upande huu wa Shia au upande wa Sunni unataja baadhi ya riwaya kutoka katika upande mwingine, ili kulitia hatiani kundi hili, pamoja na kwamba riwaya zilizopokelewa ni shadha na zisozokubalika na wengi wa maulamaa wake, lakini kwa ajili ya kuthibitisha msuguano na kuthibitisha mzozo mtu analeta mfano wa riwaya hizi na mfano wa maneno haya, ambayo ni wajibu ummah uyavuke na tuyavuke kwenye mijadala.

Kama ambavyo namuunga mkono Dr. Khalil kwamba mjadala ni kwa ajili ya kutafiti sehemu za ushirikiano baina ya Suni na Shia, nazo ndio nyingi zaidi; hakika tofauti sio nyingi isipokuwa ni kiasi kidogo, na ni katika baadhi ya matawi na sehemu. Ama vitu vya msingi Waislamu wote wanaafikiana juu yake, ni wajibu tuthibitishe sehemu hizi za ushirikiano ambazo tunaafikiana juu yake, na lengo la mjadala sio kuhubiri madhehebu, itaninufaisha nini kupata baadhi ya watu kutoka katika Usunni ili wawe Mashia? Au Sunni kupata baadhi ya watu kutoka Shia ili wawe Masunni? Sisi tunashuhudia namna gani watoto wetu - Sunni na Shia - wanavyoishi katika hali ya kushangazwa na Wamagharibi na ustaarabu wa Kimagharibi, mas'ala sio watoto wetu wawe Sunni au Shia, tatizo ni kwamba sisi sote na watoto wetu tunatishiwa na tishio la kuwa watumwa chini ya utawala wa Kimagharibi na chini ya utawala wa wengine.

Nasisitiza hapa nukta mbili:

**Nukta ya kwanza:** Kupinga kuwatuhumu watu katika dini zao, anasema (swt):



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 21 8/19/2013 12:54:24 PM

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا ضَرَبْتُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَتَبَيَّنُوا وَلَا
تَقُولُوا لِمَنْ أَلْقَىٰ إِلَيْكُمُ السَّلَامَ لَسْتَ مُؤْمِنًا

**"Enyi mlioamini! Mtakaposafiri katika njia ya Mwenyezi Mungu, basi hakikisheni wala msimwambie mwenye kuwapa Salaam: wewe si muumini."** **(Surat Nisaa: 94).**

Haisihi kwetu kuwatuhumu wengine katika dini zao, Uislamu una madhehebu, visomo vingi na mbalimbali na si vya kuzuka tu. Ushia na Usunni sio wa leo wala wa jana, bali ulikuwepo tangu zama za mwanzo za Uislamu. Kwa nini kundi hili au wafuasi wa kundi hili wawe na shaka na dini ya wafuasi wa kundi jingine? Ni wajibu tukiri mwanzo kwamba kuna madhehebu mengi na aina mablimbali za visomo, lakini vyote viko ndani ya Uislamu mmoja.

**Nukta ya pili:** Haipasi ikhitilafu kugusa haki ya uraia na haki za kibinadamu, pindi raia Masunni wanapoishi katika nchi ya Kishia kama ilivyo sasa Iran, haipasi kuvunja haki zao kama raia eti kwa kuwa tu wao ni Masunni. Na hivyo hivyo kundi la Mashia linapoishi katika nchi ya Kisuni - yaani walio wengi ni Sunni au madhehebu rasmi ni ya Kisunni - haipasi kugusa na kuvunja haki zao kwa sababu tu wao ni Shia, inapasa kulinda haki zao kama raia, wananchi waishi kwa usawa katika wajibu wao na haki zao, na vivyo hivyo hazipasi kuguswa na kuvunjwa haki za kibinadamu, kwani hali ya kidini ni hali ya kimoyo na mtu hawezi kulazimishwa kufuata imani fulani. Anasema (swt):

**"Hakuna kulazimisha katika dini; uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkataa taghuti na akamwamini Mwenyezi Mungu, hakika yeye ameshika kishiko madhubuti kisichovunjika. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mjuzi."** **(Surat Baqarah: 256).**



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 22 8/19/2013 12:54:25 PM

Kwa kweli inapasa kusisitiza mambo haya. Na hakika mimi nataraji mjadala utaendelea kwa akili iliyotulizana iliyofunguka, na ionekane hatari kubwa inayoukabili ummah wa Kiislamu.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 23 8/19/2013 12:54:25 PM

# KUCHANGIA KWA MARA YA PILI:[2]

Mimi pamoja na wengi miongoni mwa wenye ghera na umoja wa ummah huu tulitamani kwamba mzunguko huu mpya wa mjadala uwe ni bora kimaudhui na wenye mfumo sahihi zaidi kuliko mizunguko iliyotangulia katika mwezi mtukufu wa Ramadhani, ili utumikie maslahi ya ummah, na uwe karibu zaidi na radhi ya Mola Mlezi, ambaye wahyi Wake unatulingania asubuhi na jioni kwamba:

إِنَّ هَٰذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُونِ

**"Hakika ummah wenu huu ni ummah mmoja, na mimi ni Mola Wenu kwa hivyo niabuduni."** **(Surat An'biyaa: 92).**

Na anasema (swt):

وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا

**"Na Shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarikiane."** **(Surat Aal Imran: 103).**

Na anasema:

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ وَلَا تَنَازَعُوا فَتَفْشَلُوا وَتَذْهَبَ رِيحُكُمْ ۖ
وَاصْبِرُوا ۚ إِنَّ اللَّهَ مَعَ الصَّابِرِينَ

[2] Katika kuchangia usiku wa pili 24 Dhul-Qaad 1423 sawa na 27 Januari, 2003.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 24 8/19/2013 12:54:25 PM

**"Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, wala msizozane, msije mkavunjika moyo na zikapotea nguvu zenu, na subirini; Hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaosubiri."** **(Surat An'faal: 46).**

Na hususan sisi sasa hivi tupo karibu na msimu mtukufu wa Hija, ambao ni kutilia mkazo mwonekano wa umoja wa ummah huu pamoja na kutofautiana koo zao, utaifa wao na madhehebu yao. Lakini kwa masikitiko ni kwamba mzunguko huu nao umetumbukia kwenye kasoro mbaya za mzunguko uliopita, ambapo mazungumzo yake yamechukua mwelekeo wa kuchochea chuki na hisia mbaya na kusambaza sifa mbaya za yale yaliyopokewa katika hazina za Sunni na Shia, miongoni mwa riwaya na misimamo mikali yenye kuvuka mipaka iliyotokana na sababu za kisiasa, na mielekeo ya kasumba kutoka kwa pande mbili.

Hakika mimi nataraji kwa wasimamizi wa mjadala kufanya juhudi kubwa za kimakusudi kabisa kudhibiti mwelekeo wa mjadala, na ninapendekeza wategemee fikira za Dr. Khalil bin Abdillah al-Khalil, mjumbe wa bodi ya ukufunzi ya Chuo Kikuu cha Imam Muhammad bin Suud, ili ziwe ni nguzo ya mfumo wa mjadala, na wasitoe mwanya wa kuchochea mfarakano na bughudha kutoka upande wa Sunni wala Shia, kama vile kumkufurisha yeyote miongoni mwa watu wa kibla sawa awe Sunni au Shia, au kutilia shaka usalama wa nususi za Qur'ani, au kuutuhumu Uislamu wa Maswahaba watukufu, au kutuhumu shakhsiya ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (saww), haya ni maneno mabaya yanayotia kinyaa, ambayo ni wajibu kila Mwislamu kujiepusha nayo. Kwa nini yanachochewa kupitia katika kipindi hiki cha runinga ambacho kinashuhudiwa na mamilioni ya watu ulimwenguni (wakiwemo maadui na wenye mapokezi ya sura mbaya juu ya Uislam)?

Hakika tatizo kubwa la baadhi ya mijadala na uchangiaji katika mazungumzo ni kutokana na hali ya kujikweza na kudai upande



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 25 8/19/2013 12:54:25 PM

huu au ule kwamba wenyewe ndio asili, na kwamba mwingine amezuka tu na kujichomeka, na kwamba yeye ndio upande wenye mamlaka ya kuidhinisha Uislamu wa huyu na ukafiri wa yule. Al-hamdulillahi, Sunni na Shia wote ni Waislamu, na upande mmoja hauhitaji kupata ushahidi wa uzuri wa mwenendo au kibali cha usafi wake na kusamehewa kutoka upande mwingine. Inapasa ku-vuka mantiki hii ya kiburi na kujikweza. Kisha kwa nini mjadala uchukue mwelekeo wa kuhukumiana kana kwamba kila upande unamhukumu mwingine na unatafuta ushahidi wa kumtia hatiani! Hakika hata katika mahakama huondolewa adhabu kwa shaka, kwa nini kuwepo ung'ang'anizi juu ya kupembua na kutafuta katika rundo la hazina za zamani ili kuzua shaka inayomtia hatiani Sunni au Shia?

Hapa nataja mfano mmoja kuhusu yaliyotajwa jana: "Kwamba Sayyid al-Khuiy anaona ukafiri wa asiyekuwa Shia." Hakika ni uzushi ulio wazi, maneno aliyoyanukuu msemaji jana yamekatwa, hakika Sayyid amejadili mas'ala haya katika kitabu chake *at-Tanqi-yhi Fiy Sharhil-Uruwatil-Wuthqaa* kitabu cha twahara juzuu ya pili Uk. 83 hadi Uk. 87, na ametaja kauli ya wenye kuwakufirisha wale wenye kuwakhalifu Shia, kisha akaijibu kwa hoja na dalili, na aka-malizia na natija ifuatayo: Amesema kwa tamko lake:

**"Hakika yanayotegewa katika Uislamu, katika kuhifadhi damu, kurithiana na kujuzu ndoa, ni kushuhudia kwamba hakuna mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu na kwamba Muhammad ni Mtume wake, nayo ndio kauli ya watu wengi, na hivyo Uislamu hauzingatiwi kwa sifa nyingine isiyokuwa shahada mbili, hivyo hakuna nafasi pamoja na hayo ya kuhukumu Uislamu wa walio kinyume."**

Kisha anamjibu mwenye kuamini ukafiri wa asiyekuwa Shia, eti kwa sababu tu wao wanapinga *Wilayat* ya Ahlul-Bait (as), kwa ma-neno yake anasema:



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 26 8/19/2013 12:54:25 PM

**“**Wilayat **iliyo dharura, hakika ni** Wilayat **kwa maana ya kupenda, na wao - yaani Sunni - hawapingi maana hii bali wanadhihirisha mapenzi yao kwa Ahlul-Bait. Ama** Wilayat **kwa maana ya ukhalifa, sio dharura kwa upande huu, bali ni mas’ala ya kinadharia, na wameshaitafsiri kwa maana ya mapenzi na kupenda, hata kama ni kwa kufuata wahenga wao na maulamaa wao. Ndio** Wilayat **kwa maana ya ukhalifa ni katika dharura ya madhehebu na sio dharura ya dini.”**

Kwa nini anakata maneno na anayakanganya kwa ajili ya kuchochea mas’ala ya kukufurisha baina ya Waislamu? Inatupasa tuzuie njia hii na kila upande utafute mambo na sehemu ambazo unaziona ni salama katika upande wa mwingine ili kuzishajiisha na kuzikuza badala ya kutafuta sehemu mbaya ambazo ni wajibu kushirikiana ili kuzivuka na kuondokana nazo.

Ndugu zangu watukufu, ninawausia pamoja na kuiusia nafsi yangu kumcha Mwenyezi Mungu katika umoja wa ummah huu, na katika kuhifadhi yaliyobakia miongoni mwa utukufu wake. Na hivi sasa unakabiliwa na changamoto hatari zaidi katika historia yake ikiwa ni pamoja na mapambano ya kitamaduni. Na kama kudhibiti mijadala ni jambo lisilowezekana, basi natamani kuusimamisha kwa ajili ya kujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwa ajili ya kutumikia maslahi ya ummah.

# KUCHANGIA KWA MARA YA TATU:[3]

Mijadala hii na misuguano hii daima inawaweka Waislamu mbele ya changamoto kubwa katika zama hizi, nayo ni uwezo wao wa kuivuka sehemu mbaya iliyopo katika hazina zao.

Ummah una hazina kubwa inayojumuisha vitabu vya Hadith, Fiqihi, Tarikh, na Adabu, na humo mna mengi miongoni mwa hazina za kheri na chemchem za nguvu, na inawezekana kabisa kwa Waislamu kupata mafanikio mazuri kwa ajili ya nafsi zao na kwa ajili ya wanadamu wote, kama tu, watachukua zawadi hii nzuri kutoka kwenye hazina yao. Kama ambavyo katika hazina hii, ukiacha nususi za kisharia zilizothibiti, kuna yale yanayoakisi utekelezaji wa kibinadamu katika kufahamu nususi, katika kutoa tafsiri yake, na katika matukio ya kihistoria.

Nasema, katika hazina hii kuna sehemu nyingi zenye kasoro, na hususan katika yale yanayohusiana na msimamo wa mtu kwa mwingine anayetofautiana naye kidini au kimadhehebu au kisiasa. Kwa Waislamu wote, Sunni na Shia, zimerundikana rai za kiitikadi, kifiqihi na kihistoria kuhusu wenzao, ima ni kutokana na nususi ambazo usahihi wake haujulikani na haujathibiti, au kutokana na ufahamu usiokuwa sahihi na makini wa nususi, au kutokana na ufahamu wa ugomvi na mizozo kupitia mizunguko ya kihistoria, na ambayo inateka fikira na tamaduni za wenye kukinzana.

Na je sasa Sunni anataka kumhukumu Shia kwa yote yaliyomo katika hazina yao miongoni mwa misimamo isiyofaa dhidi ya Sunni? Je Shia anataka kumhukumu Sunni kwa yote yaliyomo katika hazina yao miongoni mwa nadharia na vitendo vilivyo dhidi ya Shia? Hivyo basi hakika hisabu itakuwa ndefu baina ya pande mbili, ka-

[3] Ilikuwa usiku wa Jumatano mwezi 26 Dhul- Qaad 1423 sawa na 29 Januari, 2003.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 28 8/19/2013 12:54:25 PM

dhia itahitaji miaka mingi. Hakika mimi napendekeza mjadala uwe ndani ya duara la mustakabali na katika yale ambayo inapasa yawe, na sio kuhusu yaliyopita na yaliyoandikwa na mwanachuoni yule au aliyofutu faqihi fulani, au yaliyozungumzwa na riwaya fulani.

Namna gani sasa inapasa mtazamo wa Sunni uwe kwa Shia, na namna gani sasa mtazamo wa Shia uwe kwa Sunni? Na sio yaliyozalishwa na muda uliopita miongoni mwa matukio yaliyokusanywa na vitabu vya Sunni na Shia, na fatwa za maulamaa wao waliotangulia. Na ni yapi maeneo ya ushirikiano ambayo yanakutanisha pande mbili, kwa sasa hivi, kupitia mtazamo na ijtihadi za kileo, na sio kwa msingi wa kuchochea na kuiga waliotangulia? Je, kuna maslahi ya kidini na kidunia hata moja wanayopata pande mbili ili kuyatumikia au hakuna?

Ndugu wapenzi na ndugu zangu katika njia ya Mwenyezi Mungu, Sunni na Shia, hakika Sunni na Shia leo hawana hiyari ya kuchagua baina ya utawala wa Abu Bakri na Umar au utawala wa Ali na Husain, lakini wao wako mbele ya utawala wa Mmarekani na mamlaka yake, na meli hizi za kivita zinazosogelea nchi zetu na zinataka kulazimisha amri zake na maamuzi yake, katika mfumo wa utawala katika nchi yetu, na katika mfumo wa elimu, na harakati za jumuiya za kheri, katika mambo ya wanawake na mfano wake.

Alikwishasema mmoja wa Maulamaa wa Kiislamu warekebishaji kabla ya karne na nusu: "Bado tungali tunazozana je, Abu Bakr ni khalifa au Ali ndio khalifa hadi Samiy mwakilishi wa Uingereza akawa ndio khalifa! Na bado tungali tunajadili katika udhu juu ya kuosha mguu au kupaka mguu, hadi hatujabakia na sehemu ya kuweka mguu katika Mashariki ya kati."

Katika upande mwingine hakika sehemu zenye kasoro zilizopo katika hazina zetu sote, zinatengeneza hatari dhidi ya mustakabali



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 29 8/19/2013 12:54:25 PM

wa watoto wetu na maendeleo yetu ya kidini, ambapo akili zao zenye kufunguka juu ya mabadiliko ya kielimu na zama hazikubali tena rai za ukandamizaji na fikira za mabavu, na mapokezi mabaya.

Hakika kupakwa matope sura ya Uislamu, sura ya Nabii wa Uislamu, sura ya Ahlul-Bait na sura ya Masahaba kunatokana na baadhi ya yale yaliyomo katika hazina ya Waislamu, kwani Albabiyah na Bahai wametumia baadhi ya hazina za Kishia, na maandishi ya kutia shaka ya kileo ambayo yameandikwa na watu wanaojinasibisha na familia za Ahlus-Sunna, hakika watu hao wametumia baadhi ya yale yaliyomo katika hazina ya Kisunni. Kitabu maarufu katika kutia shaka utume wa Nabii chenye jina *as-Shakhsiyyah al-Muhamadiyyah*, na kitabu cha Fatima al-Murnisiy ambacho kinawakosea adabu wake wa Mtume (saww) chenye jina *al-Harimu Siyasiy – an-Nabiyi Wan-Nisaai*, na kitabu *Shadu Rababati Biahwali Mujtamais-Swahabati* cha Khalil Abdul-Karim ambacho kinapaka matope sura ya Maswahaba chenye juzuu tatu, vitabu vyote hivi rejea zake ni kutoka katika vitabu vya Ahlu Sunna, kama ambavyo vitabu vya Bahai na Albabiyah rejea zake ni kutoka katika vitabu vya Kishia.

Na hii inamaanisha kwamba ni wajibu kwa Suni na Shia wachambue na wapembue hazina zao za Kiislamu na waandike na kueleza upya kwa sura inayofaa, na watoe tafsiri inayoafikiana na wakati. Na sio washughulikiane wao kwa wao na kubakia kuwa ni mateka wa kasoro zilizopokelewa katika hazina zao.

Na haya ndio tunayoyatarajia kuchangia katika kufanikisha mijadala hii, na sio kuzamia katika kasoro kwa ajili ya kuchochea moto na kujizingira ndani yake na kuchomoa silaha katika mapambano ya kimadhehebu.

Mwisho natoa zawadi riwaya hii kutoka katika kitabu cha *Biharul-An'war* cha Sheikh al-Majilisiy kama mfano mzuri katika



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 30 8/19/2013 12:54:25 PM

hazina zetu na ambayo inapasa baadhi ya riwaya zenye mwelekeo mbaya wa mwenye kushadadia zisituzuie kuifanyia kazi.

Kutoka kwa Abi Abdillahi kutoka kwa wahenga wake kutoka kwa Ali amesema: "Hakika pepo ina milango nane: Mlango mmoja miongoni mwayo wataingia Manabii na Wakweli, na mlango mwingine wataingia Mashahidi na Wema, na milango mitano wataingia wafuasi wetu na wanaotupenda sisi, na mlango mmoja miongoni mwayo wataingia Waislamu wengine kati ya anayeshuhudia kwamba hakuna Mungu isipokuwa Mwenyezi Mungu na wala katika moyo wake hapakuwa na chembe ya kutuchukia sisi Ahlul-Bait."[4]

4 Al- Majilisiy: Muhammad bin Baaqir al-Anuwaar, Juzuu 79, uk. 159.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 31 8/19/2013 12:54:25 PM

# JE, TOFAUTI YA MADHEHEBU INAZUIA KUOANA?

Tofauti ya madhehebu na kuwepo na rai nyingi sio jambo jipya lililozuka katika maisha ya Waislamu, mizizi ya ikhtilafu hii ya kimadhehebu imeanza katika miongo ya kwanza, karne ya kwanza katika historia ya Kiislamu, ambapo zilidhihiri kati ya Maswahaba rai zenye kutofautiana kuhusu uongozi na ukhalifa baada ya kufariki Mtume (saww). Imam Ali bin Abu Talib (a.s.) alikuwa anaona yeye ndiye anayefaa zaidi kwa ukhalifa akiwa pamoja na Bani Hashim na kundi kati ya Maswahaba, wakati ambapo Abu Bakri alipewa kiapo cha utii katika ukumbi wa Saqifa ya Bani Saa'idah, huku Ali akiwa hayupo pamoja na wanaomuunga mkono.

Pamoja na kwamba Imam Ali (a.s.) na aliokuwa pamoja nao baadaye walimpa kiapo cha utii Abu Bakri isipokuwa ni kwamba mwelekeo wa wafuasi wa Ahlul-Bait (as) wanaitakidi kwamba wao ndio wanaostahiki na wana haki zaidi. Kisha ukaja utawala wa Bani Umayya na hatimaye yale yaliyotokea humo ikiwa ni pamoja na Ahlul-Bait na wafuasi wao kukandamizwa. Kilele chake kikafikia katika tukio la Karbalaa mwaka 61 Hijiria, na ukaimarisha mwelekeo wa kuwapenda na kuwafuata Ahlul-Bait katika ummah. Na hapo ikatofautiana mielekeo miwili, mwelekeo wa jumla na rasmi, na ambao baadaye ulipewa jina la Ahlu Sunna Wal–jamaa, na upande unaofuata Ahlul-Bait na ambao baadaye ulijulikana kwa jina la Shia.

Kama ambavyo ulidhihiri mwelekeo wa tatu katika ukhalifa wa Ali (as) kutokana na tukio la tahkim katika tukio la Sifin, nao ni mwelekeo wa Khawarij ambao walipinga tahkim baada ya kutokea kwake, wakaasi utawala wa Imam Ali (as).



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 32 8/19/2013 12:54:25 PM

Mieleko yote hii iliimarisha mwonekano wake katika nusu ya kwanza ya karne ya kwanza Hijiria, na katikati ya karne ya pili ilianza kudhihiri madrasa za kitheiolojia na madhehebu za kifiqihi, kama vile madrasa ya Ahlul-Hadith, watu wa rai binafsi, Ashairah, Mu'utazilah na madhehebu mengine ya Ahlus Sunna, na mielekeo ikawa mingi kwa wafuasi wa Ahlul-Bait (as).

Na kwa kupita muda, na kutokana na sababu za kisiasa na mtazamo wa ushindani na utafiti wa kielimu, madhehebu za msingi zikaota mizizi na michipuo katika ummah, na zikayeyuka au zikadhoofika madhehebu nyingine.

## WINGI KATIKA HALI YA UMOJA

Lakini wingi wa madhehebu na mitazamo katika karne hizo za mwanzo haukuathiri katika Umoja wa Ummah, na haukutengeneza vizuizi vya kijamii baina ya wafuasi wa madhehebu na mitazamo hiyo. Hiyo ni kwa sababu misingi ya Kiislamu katika dini na mafunzo ya kimsingi ya sharia yalikuwa yanazingatiwa kuwa ni mpaka unaowakusanya pamoja na wigo wenye kuwakutanisha pamoja. Unajumuisha madhehebu mengi na mitazamo mbalimbali, wote wanaamini Mwenyezi Mungu ndio Mola, Muhammad (saww) ndio Nabii, Akhera ndio marejeo, Qur'ani ndio Kitabu, na Kaaba ndio kibla, na wanashikamana na Sunna ya Mtukufu Mtume (saww), wanasimamisha Swala kwa faradhi zake tano, wanatoa Zaka, wanafunga mwezi wa Ramadhani, wanatekeleza faradhi ya Hija katika wakati wake uliopangwa na wanaafikiana katika kuharamisha pombe, zinaa, riba na haramu zingine zinazojulikana baina ya Waislamu.

Ama tofauti za rai katika baadhi ya ufafanuzi wa itikadi na fiqihi au kutofautiana misimamo ya kisiasa haisihi kuubadili umma na kuwa



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 33 8/19/2013 12:54:25 PM

ni kundi linalojitenga mbali na wengine. Na kuoana na kuchanganyika koo na kabila ilikuwa ni mwonekano kati ya mwonekano wa umoja wa jamii ya Kiislamu na mshikamano wake ambapo tofauti hazikuwa ni kizuizi dhidi ya hilo, lakini mazingira ya kushambuliana kimadhehebu ambayo ummah uliyaishi baada ya hapo yameleta mwelekeo wa kutengana na kuwa mbali kijamii baina ya wafuasi wa madhehebu, hivyo zikatokea fatwa za kukufurishana na kuharamisha kuoana baina ya Waislamu, pale yanapotofautiana madhehebu yao.

## MWISLAMU MWANAMUME ANAFAA KWA MWISLAMU MWANAMKE

Mafakihi wanatia mkazo kwamba asili ya kujuzu kuoana baina ya Waislamu pamoja na kutofautiana madhehebu yao, Mwislamu mwanaume anafaa kwa Mwislamu mwanamke. Amesema al-Muhaqiq al-Hilliy (aliyezaliwa mwaka 602 na kufariki mwaka 676 Hijiria) katika Sharaiul-Islaami: "Al-Kafaatu ni sharti la ndoa, nayo ni kulingana katika Uislamu, je kunashurutishwa kulingana katika imani? Humo kuna riwaya mbili, iliyo dhahiri zaidi ni kufaa kwa Uislamu hata kama kuna kutia mkazo katika sunna ya imani, na hususan katika upande wa mke, kwa sababu mwanamke anafuata dini ya mume wake."[5]

Na amesema Sheikh Muhammad al-Hasan Najafiy katika *al-Jawahir* baada ya kujadili kwake rai na riwaya ambazo kidhahiri inaonekana ni kuzuia kuoana baina ya Shia na Sunni na wengineo, amesema kwa kauli yake: "Lengo la Uislamu katika ndoa, hakika makundi yake yote ambayo haijathibiti ukafiri wake kwa nasibi (uadui) au ghuluu au mfano wa hayo ni mila moja tu, wanashirikiana

[5] Al-Hilliy: Ja'far bin Hasan katika *Sharaiul- Islami* kitabun nikaahi lawaahiqil-Aqdi mas'ala 1



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 34 8/19/2013 12:54:25 PM

katika kuoana na kurithiana na yasiyokuwa hayo kati ya hukumu na adhabu."[6]

Na amesema Sheikh Muhammad Jawadi Mughuniya: "Kulingana baina ya wanandoa kwa Shia Imamiya ni Uislamu na unatosha kuwa ni makutano bila ya kujali tofauti baina ya madhehebu ya Kiislamu na makundi yake yote."[7] Na imekuja katika Sahihi Abdillahi bin Sanan amesema: "Nilimuuliza Abi Abdillahi as-Sadiq (as): Kwa kitu gani mwanaume Mwislamu anakuwa halali kumuozesha na kumrithisha, na kwa kitu gani inaharamishwa damu yake? Akasema (as): 'Inaharamishwa damu yake kwa Uislamu, na unapodhihiri inakuwa halali kumuozesha na kumrithisha.'"[8] Na kutoka kwa Qasim as-Swairafiy Sharik al-Mufadhwal amesema: "Nilimsikia Abu Abdillahi (as) anasema: 'Kwa Uislamu inahifadhiwa damu, na kwao inatekelezwa amana, na kwao inahalalishwa tupu na malipo ni kwa imani.'"[9]

Na imekuja katika *Fiqihu-Sunnah* kutoka kwa Ibnu Hazim kauli yake: "Mwislamu yeyote maadamu hakuwa mzinifu ana haki ya kumuoa Mwislamu yeyote mwanamke maadamu hakuwa mzinifu, na Waislamu wote ni ndugu." Kama ambavyo amenukuu kutoka kwa as-Shaukaaniy kauli yake: "Mazingatio ya kulingana katika dini ni asili na ukamilifu, hivyo Mwislamu mwanamke haolewi na kafiri, wala mwenye heshima haolewi na muovu, na Qur'ani na Sunnah hazikuzingatia katika kulingana jambo lingine zaidi ya hilo, hakika imeharamishwa Mwislamu mwanamke kuolewa na mzinifu muovu."[10]

---

[6] Najafiy: Sheikh Muhammad Hasan katika Jawahirul-Kalaami Juzuu 10, uk: 681

[7] Mughuni: Sheikh Muhammad Jawad katika *Fiqihi al-Imama Ja'far Swaadiq*, Juz. 5, uk: 216.

[8] Al-Hurru al-A'amilliy: Muhammad bin Hasan katika Wasailus-Shi'ah - Hadithi ya 26333 – kitabu nikaahi.

[9] Rejea iliyotangulia hadithi namba 26337.

[10] Saabiq: Sayyid Saabiq katika *Fiqihus Sunnati* Juz. 2, uk. 143-146 chapa ya 3 ya 1977 Darul- kitaabil-Arabiy

## HOFU YA KUATHIRIKA:

Kwa sababu watu wa kila madhehebu wanazingatia kwamba madhehebu yao ndio haki na sahihi zaidi, basi hakika wao wanajali kitendo cha kuwaepusha watoto wao na mazingira ambayo yanawazuia wao kuambatana na madhehebu yao, na haya ndio yanayoashiriwa na baadhi ya fatwa za mafaqihi kwa anwani ya hofu ya kupotea au kuwepo kwa uharamu. Anasema Sayyid Shiraziy katika jawabu lake juu ya swali: Je, inajuzu kwa mwanamke wa Kishia kuolewa na mwanaume wa Kisunni? Jawabu: Ilivyo mashuhuri ni kwamba inajuzu isipokuwa kama kuna ubaya mwingine, kama itajulikana kwamba yeye atamlazimisha kujiepusha na Ahlul-Bait (as) au kwamba yeye hatomruhusu kufanya amali zake na ibada zake kwa mujibu wa madhehebu yake."[11]

Anasema Sayyid Sistaaniy: "Inajuzu kumuozesha muumini kwa mwanamke asiyekuwa wa madhehebu yake asiye kuwa Nasibi (adui) kama ambavyo inajuzu kumuozesha mwanamke muumini kwa mwanaume asiyekuwa Nasibi (adui) ijapokuwa ni makuruhu, na ni haramu kama itahofiwa kuwa mwanaume au mwanamke atapotea."[12] Na amenukuu Ibn Abi Qudaamah al-Hanbaliy katika *al-Mughuniy* kutoka kwa Imam Ahmad bin Hanbali kauli yake: "Haozeshwi binti kwa Haruriy aliyeasi katika dini wala kwa Shia wala kwa Qadiriya, lakini ikiwa halinganii hakuna ubaya."[13]

Na kauli yake "Ikiwa halinganii hakuna ubaya" ni kuashiria kwamba kuzuia ni kwa ajili ya kuogopa kuathirika kimadhehebu. Mas'ala yanafungamana na mazingira salama ya kuamilina,

---

[11] Shiraziy: Sayyid Muhammad katika *Ajuwibatul-Masaaili shari'iyati* – yaliyoandaliwa na Sheikh al-Haairiy uk. 132 mas'ala ya 461.

[12] Sistaaniy: Sayyid Ali al-Husainiy katika Minhaaji swaalihiyna juzuu 3 uk: 70

[13] Ibnu Qudaamah al-Hanbaliy: Abdillahi bin Ahmad katika *al-Mughuniy* Juz. 9, uk. 397 chapa ya pili 1992 Cairo



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 36 8/19/2013 12:54:25 PM

kuheshimiana na kubadilishana, kuzuia na kujilinda kuliopo ni kwa sababu ya uhusiano usio wa kawaida baina ya wafuasi wa madhehebu, lakini hali nzuri inapotawala basi hakutakuwa na kisingizio cha kuzuia na kujilinda.

## MAKUNDI YANAYOONDOLEWA:

Na mafaqihi wa Kishia wameyaondoa baadhi ya makundi kwa kuharamisha kuoana pamoja nayo, hata kama wanadhihirisha Uislamu, nayo ni:

1. *Al- Ghulaati* ambao wanaitakidi kwamba kuna mmoja kati ya binadamu ana sifa za uungu, kama vile *Maghulaati* wanaompandisha Imam Ali au Ahlul-Bait katika daraja ya uungu, wao kwa mafaqihi wa Kishia wanahukumiwa kuwa ni najisi na makafiri.
2. *Nawasibi* nao ni wale wenye kutangaza uadui kwa Ahlul-Bait na umaasumu wao, lakini wao Ahlul-Bait hawawachukii wala hawawafanyii uadui.
3. *Khawaariji* ambao wanatangaza chuki kwa Imamu Ali (as), ama Khawariji ambao wamejiunga na madhehebu yao bila ya kudhihirisha uadui au chuki kwa Ahlul-Bait basi wao wanahukumiwa kuwa ni Waislamu. Kama hali ilivyo kwa Maibaadhi wa Oman kulingana na tunavyowajua.*

## KULETA MKURUBA (UKARIBIANO) BAINA YA WAFUASI WA MADHEHEBU

Katika kujitolea kuzuri ambako kunastahiki shukurani na heshima, jarida la kila wiki la Madina limetenga kurasa mbili katika toleo lake



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 37 8/19/2013 12:54:25 PM

tarehe 23 Jumadil-Ulaa 1422 Hijiria kwa ajili ya kujadili mas'ala ya kuleta mkuruba baina ya Sunni na Shia chini ya kichwa "ar-Risalah," na limewashirikisha katika utafiti wa maudhui hii maulamaa na wanafikira watukufu wa Sunni na Shia kutoka Saudia, Iran na Misri.

**Kutoka Saudia:**

— Dkt. Sheikh Abdillahi bin Bayyatu, mjumbe wa Baraza la Sharia ya Kiislamu huko Jiddah, na muhadhiri wa masomo ya Kiislamu katika Chuo Kikuu cha al-Malki Abdul-Aziz.

— Dkt. Sheikh Abdillahi al-Abiyd, katibu mkuu wa zamani wa Shirikisho la Nchi za Kiislamu, na mbunge wa Bunge la Saudia kwa sasa.

— Sheikh Abdillahi bin Muni'I, mjumbe wa baraza la Ulamaa wakubwa, Saudia.

— Sayyid Ali al-Musawiy, ambaye ni kati ya Ulamaa wa Hawza ya elimu ya al-Ahsaai.

**Kutoka Iran:**

— Sheikh Muhammad Waaidh al-Khurasaniy, Katibu mkuu wa Jumuiya ya Kimataifa ya Kuleta Mkuruba Baina ya Madhehebu ya Kiislamu, Iran.

— Sheikh Muhammad Yazidiy, Jaji Mkuu Mstaafu wa Iran, ambaye sasa ni mjumbe wa Baraza la kulinda Katiba ya Iran.

— Sheikh Muhammad Mahdiy al-Isfaahaniy, mmoja kati ya Maustadh wa Hawza ya elimu ya Qum.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 38 8/19/2013 12:54:25 PM

**Kutoka Misri:**

— Mufti wa Misri, Dkt. Naswir Farid Waaswil

— Dkt. Sheikh Yusuf al-Qaradhawiy, mwanachuoni na mlinganiaji maarufu

— Dkt. Muhammad Ammaarah, mwanafikra na mwandishi maarufu.

Na umuhimu wa kujitolea huku unatokana na umuhimu wa maudhui haya katika jamii ya kidini katika nchi ya Saudia, na kwa hiyo magazeti ya Saudia hayakuwa yakizungumzia utatuzi wake isipokuwa kwa kunukuu mtazamo wa upande mmoja. Na inaonekana kwamba mabadiliko na mazingira mapya ndio yameshajiisha dhamira ya kuwasilisha maudhui haya kwa ujasiri wa kielimu, na kwa njia ya kimaudhui inayokusanya rai za pande zote na inayotatua mas'ala kwa uzuri na uwazi bila ya kushambulia wala kuchochea.

Na kwa kuongezea ni kwamba, hakika mkutano wa Janadiriya ulijitolea kuelezea maudhui hii miaka miwili iliyopita, kama ambavyo jarida la *al-Watwani* la Saudia limechapisha baadhi ya makala nzuri katika maudhui haya. Na kitafuata muda si mrefu kiambatanisho cha jarida la *al-Madinah* ili kuimarisha mwelekeo wa maudhui haya katika kuwasilisha utatuzi wa mas'ala haya magumu: Uhusiano baina ya Shia na Sunni, katika wakati ambao kuna haja ya ummah kuwa na umoja, na katika medani, maadamu umekabiliwa na upweke na mashambulizi ya kimadhehebu.

**Kuleta mkuruba baina ya madhehebu au wafuasi:**

Kabla ya miaka hamsini wanachuoni wawili wema kutoka katika



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 39 8/19/2013 12:54:26 PM

Sunni na Shia walijenga maudhui ya kuleta uelewano baina madhehebu ya Kiislamu, nao ni Sheikh Muhammad Taqiy al-Qummiy kutoka Iran na Sheikh Mahamud Shaltut Sheikh wa Al-Azhari wakati huo, na ikaundwa taasisi huko Cairo ya kusimamia suala hili, kwa jina la Daru Taqriyb Bainal Madhaahibil-Islamiyat, na ikatekeleza jukumu zuri la kihistoria, lakini harakati zake zilisimama baadaye kwa sababu za kisiasa, na kabla ya miaka kadhaa uongozi wa kidini wa Iran uliamua kurejesha upya harakati na shughuli katika nyanja hii, kupitia taasisi kwa anwani ya Jumuiya ya Kimataifa ya Kuleta Mkuruba Baina ya Madhehebu ya Kiislamu (al- Majmaul-A'lamiy Lil-itaqrib Bainal-Madhahibil-Islamiyati). Na katika upande wa kimtazamo hakika anwani ya kuleta ukaribu baina ya madhehebu ya Kiislamu sio makini:

**Kwanza:** Hakika madhehebu ya Kiislamu yako karibu katika asili yake na katika misingi yake ya jumla, ambapo wote wanaafikiana katika kurejea kwenye Kitabu na Sunna, na yanaamini katika msingi wa ushirikiano, nayo ni tauhidi, utume na marejeo, na yanakusanywa na nguzo za Kiislamu na faradhi zake za kimsingi, kama vile Swala, Saumu, Hija, Zaka, Kuamrisha mema na Kukataza maovu na Kupigana Jihadi katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Na ikhitilafu katika madhehebu hakika ipo katika baadhi ya ufafanuzi na matawi na ni sehemu ndogo, na hii haimaanishi kuwa yako mbali. Lakini tatizo linatokana na yaliyotokea katika ummah katika zama za nyuma, kwa kutilia mkazo nukta chache za ikhitilafu na kusahau maeneo mengi ya mwafaka. Anasema Dkt. Husain Ali Mahfudh, naye ni mwanachuoni mtafiti kutoka Iraki: "Nimesoma vitabu vya fiqhi na nimesoma mas'ala ya kuhitalafiana, nayo ni mas'ala 4152 katika jumla ya mas'ala mengi ya kifiqhi ambayo

* *Durusu fiyl-Usurati* – darsi namba 21 tarehe 1, Rabiul-Awwal 1422 Hijiria



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 40 8/19/2013 12:54:26 PM

katika baadhi ya vitabu yanafikia mas'ala 160,000, sijaona mas'ala katika madhehebu na wala sijakuta rai katika kundi, isipokuwa rai hiyo imesemwa (pia) na kundi la mafaqihi (wa madhehebu nyingine) au imesemwa na baadhi ya jamaa miongoni mwao au imepokewa kutoka kwa watu fulani. Na nimehakiki mas'ala ambazo baadhi ya madhehebu yamepwekeka nayo nikakuta ni mas'ala 253 tu kati ya mas'ala zenye ikhitilafu baina ya madhehebu, na sio katika jumla ya mas'ala zote za fiqhi. Na kama tutasoma vitabu vya fiqhi na hukumu tutakuta (mas'ala) zipo katika mkondo mmoja takriban, kwa lugha ya kifiqihi yenye kushirikiana, zinakaribiana katika matamko na mnyumbuliko."[14] Madhehebu yanakaribiana na wala haihitaji kuyafanya yawe karibu.

**Pili:** Anwani hii inaweza kuleta hofu na kikwazo kwa baadhi ya watu kwamba mkuruba baina ya madhehebu inamaanisha kutanazali na kuacha baadhi ya rai na mambo ambayo wana ukinaifu nayo ili tukutane katika nukta ya kati. Na baadhi wametangaza kuwa waangalifu na fikira ya kuleta mkuruba baina ya madhehebu kutokana na kikwazo hiki. Na dhahiri ni kwamba kinachotakiwa si mtu kupitia sifa ya mazungumzo au muamala mzuri aachane na jambo la kidini la kimsingi ambalo ana yakini nalo kihoja, sawa iwe katika mas'ala ya kiitikadi au kifiqihi. Kisha hakika madhehebu yatabaki katika mitazamo yake na rai zake na ijtihadi zake, hivyo nini maana ya kuleta mkuruba baina yake?

Ilivyo sahihi zaidi ni anwani iwe kuleta mkuruba baina ya wafuasi wa madhehebu ambao udhaifu wao wa uelewa wa dini umewaweka mbali, na tabia ya kasumba, kuvuka mpaka, uwepo wa malengo ya kimaslahi binafsi katika ikhitilafu na njama za maadui za kuusambaratisha ummah vimewasambaratisha. Na kana kwamba Imam Ali

[14] Jawad: Ghaanim katika *Nahawa Thaqaafati Taqriyb bainal-Madhaahibil-Islamiyati*/ jaridatu-hayaati toleo la 4 Shaaban 1421Hijiria.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 41 8/19/2013 12:54:26 PM

bin Abu Talib (as) alikusudia hali hii katika kauli yake katika moja ya khutuba zake: “Hakika nyinyi ni ndugu katika dini ya Mwenyezi Mungu, hafarakishi baina yenu isipokuwa mwenye nia mbaya na mwenye dhamira mbaya, hivyo hamtosaidiana, hamtopeana nasaha, hamtoshirikiana wala hamtopendana.”[15]

Inadhihirika kwamba kwa hakika haya ndio makusudio ya mkuruba wowote baina ya wafuasi wa madhehebu, lakini anwani haielezi hilo kwa kina na uwazi.

**Jukumu la maelekezo ya kidini:**

Alhamdulillahi, Ummah wa Kiislamu umevuka hatari nyingi za kugawanyika kikabila na mizozo ya kinchi, na hata kama hayo yanatokea katika baadhi ya nyakati isipokuwa ni kwamba ni ndani ya mpaka wa kimaslahi na usiokuwa na mashiko katika nafsi za watu wa ummah uliotosheka na misingi ya Uislamu. Lakini hatari kubwa juu ya umoja wa ummah huu leo inapatikana katika ikhitilafu za kimadhehebu na kimakundi, kwa sababu zinatokana na mazingira ya kidini kulingana na uwelewa wa watu wake kuhusu dini, na kwa sababu zina mizizi ya kinafsi na kihistoria ya kina.

Na hapa inakuja nafasi ya maelekezo ya kidini, kwani yanaweza kufanya kazi ya kuunganisha safu, kuondoa mpasuko, na kuwaleta karibu watu wa ummah pamoja na kutofautiana madhehebu yao, ili kukabiliana na changamoto za pomja, na hatari zinazonyemelea dini na ummah, na kuwakumbusha Waislamu misingi inayounganisha, na misingi mikuu ambayo wanatokana nayo. Na hiyo ni kama tu maelekezo haya yametoka kutoka upande wenye kuelewa wenye kufahamu malengo ya dini na maslahi ya ummah.

[15] Al-Musawiy: Sharifu Ridhwaa katika *Nahjul-Balaghah* khutuba ya 113.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 42 8/19/2013 12:54:26 PM

Na baadhi ya maelekezo ya kidini yanaweza kutekeleza jukumu baya kwa kutilia mkazo mambo ya ikhtilafu na kuushughulisha ummah na mambo ya pembeni na matukio ya kihistoria, na kuwahamasisha watu wake dhidi ya wengine wenye kutofautiana nao kimadhehebu, kwa kutoa fatwa ya kukufurisha na matangazo ya bidaa na ufasiki, na kuwagawa Waislamu kwa misingi mibaya ya kiubaguzi na kikabila, baina ya watu wa nchi moja kutokana na ikhtilafu za kimadhehebu.

Medani ya Kiislam imekabiliwa sana na uvukaji mipaka na msuguano wa baadhi ya maelekezo ya kidini, na ambayo yametengeneza kizazi cha wenye kasumba wenye kuchupa mipaka, ambao wamepaka matope Uislamu na wamezua fitina na mparaganyiko katika jamii zao, na yanayotokea Nigeria, Afghanistan na Pakistani hakika ni matokeo na matunda ya mwelekeo huu na maelekezo haya yenye kuchupa mipaka.

**Da'awa ya kuleta mkuruba ni namna gani itafaulu?**

Da'awa ya kuleta mkuruba imeanza Misri na Iran na ikaungwa mkono na pande na harakati za Kiislamu toka nchi mbalimbali, na imekata masafa mazuri kuelekea katika malengo yake mazuri, lakini haijapata mafanikio yanayotakiwa na haijafikia kwenye lengo linalotarajiwa. Na itakidi yangu ni kwamba Serikali ya Saudi Arabia kwa uzito iliyonao kimataifa na nafasi iliyonao katika Ulimwengu wa Kiislamu, na kwa uwezo iliyonao wa kimaada na kimaanawi, inaweza kucheza dauru kubwa yenye mafanikio katika kufanikisha da'awa ya kuleta mkuruba baina ya wafuasi wa madhehebu za Kiislamu.

Na kama ambavyo Serikali ya Saudia ilikuwa na mchango mkubwa wa kuunganisha nchi za Kiislamu katika mkutano wa



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 43 8/19/2013 12:54:26 PM

Jumuiya ya Nchi za Kiislamu, na kutokana na jaribio la Wazayuni kuchoma Masjid al-Aqswaa tarehe 21 Agosti 1969, Serikali ya Saudia ilifanya juhudi kubwa ya kufanyika mkutano wa kwanza wa Kiislamu, na kwa msingi wake ikaanzishwa Jumuiya ya Nchi za Kiislamu. Na leo ambapo hasira ya Wazayuni wenye uadui inazidi na kupamba moto kwa njia ya vita vyao kwa kuvuka mipaka yote na matarajio, ambapo wananchi wa Palestina wenye kusubiri wanaingia katika vita hatari, ni haja ilioje ya ummah ya kuwa na mshikamano mzuri unaotia nguvu umoja wake na kunyanyua maanawiya ya watu wake na wapiganaji wake, na kila mmoja kuelekeza uwezo wake na juhudi zake katika kuikomboa Qudusi tukufu na kuzikomboa ardhi zilizoporwa!

Na hiyo itatimia kwa kufanikisha hatua hii ya umoja mkubwa ili kuleta mshikamano baina ya watu wa ummah huu na wananchi wake na kufunga ukurasa wa ikhtilafu baina ya wafuasi wa madhehebu za Kiislamu, Sunni na Shia, na kufunga faili baya, hususan mashujaa wenye ghera kati ya Sunni na Shia wanasimama katika msitari mmoja katika kupambana na uvamizi wa Kizayuni, kwani mapigano na ushindi wa Shia Kusini mwa Lebanon ndio ambayo yamewasha utambi wa harakati tukufu huko Palestina. Na Serikali ya Saudia kama ambavyo ilikuwa na mchango mkubwa wa kuwakusanya viongozi wa nchi zote za Kiislamu, hakika inaweza kusimamia jukumu la umoja upya kwa ajili ya kukusanya viongozi wa madhehebu juu ya msingi wa uongofu wa Kitabu na Sunna. Na tunaamini kwamba mikutano ya Janadariyah kuhusu kuleta ukaribu baina ya madhehebu za Kiislamu, ikiwa ni pamoja na yale yanayoandikwa na magazeti ya Saudia miongoni mwa maandishi na tafiti mbalimbali katika mwelekeo wake, ni ishara ya kusimamia jukumu hili muhimu.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 44 8/19/2013 12:54:26 PM

# KIAMBATANISHO FIKRA KUHUSU MJADALA BAINA YA SUNNI NA SHIA: DKT. KHALIL BIN ABDILLAH AL-KHALIL:

Majadiliano ni alama kati ya alama za maendeleo yenye nguvu yenye asili na hai, na Uislamu umelingania kufanya mazungumzo na wengine wasiokuwa Waislamu, sasa itakuwaje mazungumzo baina ya makundi na madhehebu za Kiislamu, bali Uislamu umekwenda mbali zaidi ya mazungumzo nayo ni mjadala:

ادْعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ ۖ وَجَادِلْهُمْ بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ

**"Waite kwenye njia ya Mola Wako kwa hekima na mawaidha mazuri na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora."**

**(Surat Nahli; 16:125).**

Hivyo mazungumzo yana manufaa na yana faida baina ya makundi na madhehebu, jamaa na vyama vya Kiislamu, maadamu ni wenye kujilazimisha na adabu ya mazungumzo na masharti yake na taratibu zake za kisharia na kielimu.

**Malengo ya majadiliano yenye matunda:**

Ni kila upande kujua uliyonayo upande mwingine kulingana na rai zao zilizo nyingi na za dhahiri au zinazoaminiwa ikiwezekana, bada-



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 45 8/19/2013 12:54:26 PM

la ya kulijua kundi kupitia rai zisizoaminiwa au rai zinazopuuzwa na zisizotakiwa.

Na kutokana na majadiliano Sunni atajua misingi, itikadi na hukumu za ndugu zao na wafuasi wa madhehebu ya Ja'fariya, na Shia watajua misingi na itikadi na hukumu za ndugu zao Ahlus-Sunna, kulingana na yaliyoenea, yanayopendelewa na yaliyothabiti kwa kila upande kwa wakati uliopo, pamoja na kuchunga kutokutia chumvi katika mahakama ya historia au kuhukumiana kwayo.

**Utafiti juu ya maeneo ya ushirikiano baina ya Sunni na Shia:**

Kupanga mwelekeo wa ikhtilafu baina ya Sunni na Shia katika mambo ya kimsingi, bila ya kuingia katika ufafanuzi wa matawi, na marejeo ya mpaka huu ni yale ambayo yanasemwa na kila upande juu ya madhehebu yake na sio yale yanayosemwa na kundi jingine kutokana na makosa na sababu za kihistoria, yaliyotengenezwa na matukio ya kisiasa na ugomvi wa kikabila, kinchi na kimadhehebu.

Sio lengo la mazungumzo kumtoa yeyote katika kundi ambalo anajinasibisha nalo, au kueneza shaka na propaganda na fitina katika ummah, bali lengo ni: Wafuasi wa kundi la Sunni au Shia wajue misingi yao na itikadi yao na hukumu za dini yao za kimsingi, kwa njia ya kimaendeleo, na kulinganisha na waliyonayo ndugu zao Waislamu wa kundi jingine.

Mazungumzo yanatakikana kwa Waislamu na kwa wasiokuwa Waislamu, na hivyo ni muhimu kujilazimisha na mfumo wa kielimu na ukimya wa hali ya juu, ili kutoa mfano wenye manufaa wenye kuathiri ulio hai unaotumikia kadhia ya kimsingi tunayoihitaji sote. Nayo ni kueneza moyo wa usamehevu ambao Uislamu unalingania.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 46 8/19/2013 12:54:26 PM

# MWISHO:

Sio katika malengo ya mjadala kuleta ukaribu baina ya madhehebu mbili, wala sio katika malengo yake kuunganisha baina ya madhehebu mbili, na sio katika malengo yake kushinda mjadala na mdahalo dhidi ya mpinzani na kumdharau na kuteremsha hadhi ya kundi lake ambalo analitambulisha hali ya kuwa ni mwenye kushukuriwa kwalo, na ambalo analitetea hali ya kuwa ni mwenye kulipwa thawabu kwa haki juu yake. Abadan (hilo si lengo), hapa hakuna mshindi wala mshindwa, katika majadiliano haya ya kihistoria ambayo yamefanywa na kituo cha Chanel ya al-Mustaqilah cha Runinga ya London.

Wote ni wenye kuchuma na wote ni washindi, lengo la mjadala ni kujua ukweli kutoka kwa wahusika wanaojinasibisha na kila kundi, na kutafuta maeneo ya kushirikiana na kueneza moyo wa usamehevu baina ya Waislamu pamoja na kutofautiana utamaduni wao na makundi yao, kwa elimu na uoni, na kwa mahaba na unyenyekevu, na kwa kujali heshima ya pande zote na kwa uelewano unaotakiwa, na haya yote yatatimia katika msingi wa utafiti wa kielimu wenye jitihada na bidii ya kutengeneza mazingira mazuri ya kuamiliana yenye kuafikiana na utulivu, amani na mafanikio, ili wote wachangie katika kujenga mwamko unaotakiwa, ambao utawapa saada wananchi na kuhifadhi haki, na kuwakemea wapuuzi na kuwazuia wenye tamaa na utajiri wa ummah na ardhi zake, matukufu yake na misingi yake.

Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuwafikisha na ndiye Mwongozaji katika njia ya sawa.

**Dkt. Khalil bin Abdillahi – Riyaadh,**

Mjumbe wa bodi ya ukufunzi ya Chuo Kikuu cha Imam Muhammad bin Suudi al-Islamiyah,

17 Dhul- Qaad 1423 Hijiria sawa na 19 Januari 2003.



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 47 8/19/2013 12:54:26 PM

# ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA

## AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo  Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo  Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa

17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyeezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.

39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusherehekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 50 8/19/2013 12:54:26 PM

61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 51 8/19/2013 12:54:26 PM

82. Urejeo (al-Raja'a )
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102 Hukumu zinazomhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 52 8/19/2013 12:54:26 PM

104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenye hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 53 8/19/2013 12:54:26 PM

125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali (‘a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s) (Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah

146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 55 8/19/2013 12:54:26 PM

167. Mshumaa
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu
    (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 56 8/19/2013 12:54:26 PM

188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina (‘as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwanendo wa Imam ‘Ali (‘a)
198. Kuelewa Rehma ya Mwenyezi Mungu
199. Mtazamo kuhusu msuguano wa kimadhehebu



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 57 8/19/2013 12:54:26 PM

# KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA

## KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba'Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 58 8/19/2013 12:54:26 PM

# MUHTASARI



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 59 8/19/2013 12:54:26 PM

# MUHTASARI



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 60 8/19/2013 12:54:26 PM

# MUHTASARI



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 61 8/19/2013 12:54:26 PM

# MUHTASARI



10_Mtazamo kuhusu_20_July_2013.indd 62 8/19/2013 12:54:26 PM